BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 24 Mei, 2023**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

84. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali inavyowathamini wananchi wake kwa kuwalinda na kuwajengea miundombinu mbali mbali ya barabara na mitaro ya kupitisha maji, ili wakati wa mvua za masika wasipate mafuriko na maambukizi ya maradhi. Katika jitihada hizo Serikali imeleta wakandarasi mbali mbali ili kujenga

mitaro ya kisasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia au kuunda kikosi kazi kwa ajili ya kuisafisha mitaro hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

96. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kutokana na matumizi mapana ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shughuli za kila siku, baadhi ya taasisi za Serikali kama vile ZRA (ambayo hapo awali ilikuwa ZRB) zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kushindwa kuwabagua watumishi kati ya Wahasibu, Washika Fedha na Maafisa TEHAMA, jambo ambalo linaingilia mgawanyo wa majukumu.

(a) Je, ni vigezo vipi hutumika kuwatofautisha watumishi hawa kabla na wakati wa kuajiriwa.

(b) Kwa vile mifumo ya kielektroniki imekuwa ikifanya kazi nyingi za watumishi hawa, je, ni upi mpango mpya wa ugawaji wa majukumu kwa Wahasibu, Washika Fedha na Maafisa TEHAMA kwa taasisi kama ya ZRA.

(c) Je, ZRA haioni haja ya kuanzisha chuo kwa ajili ya kuwafunza zaidi watumishi na watumishi watarajiwa kulingana na mabadiliko ya teknolojia ya sasa.

112. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Moja katika malalamiko ya wanaotathmini matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali ni gharama kubwa zisizo za lazima za matumizi ya magari yenye uwezo mkubwa na yanayohitaji matunzo makubwa yanayotumiwa na viongozi wa kawaida wa Serikali, ukilinganisha na hali duni za maisha ya watu wetu. Jambo hili linaongeza matumizi ya kawaida ya Serikali ambayo yangeweza kupunguzwa hasa ukitilia maanani barabara nyingi za Zanzibar ni nzuri na salama katika masafa ya wastani.

(a) Je, kuna sababu zipi za kiuchumi na kiusalama zinazoisababisha Serikali kutotumia magari ya daraja za kati kwa viongozi wa kawaida wa Serikali.

(b) Je, ni gharama gani Serikali hutumia kwa mwaka katika kuyahudumia magari ambayo viongozi wa kawaida wanayatumia.

(c) Je, ni upi mpango bora wa Serikali katika kupunguza gharama zinazotokana na magari ya daraja za juu kwa viongozi wa kawaida wa Serikali.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

15. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni tumeshuhudia tukio la utiaji saini wa mikataba mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Kitendo hicho ni kati ya hatua za maandalizi ya utekelezaji wa shughuli hizo. Kwa kuwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ni miongoni mwa shughuli inayotarajiwa kutekelezwa kwa mujibu wa tukio hilo.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza rasmi.

94. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Utaratibu wa nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea duniani ni kuwapa tahfifu ya nauli ya usafiri wanafunzi wa skuli za msingi, sekondari na vyuo. Kwa bahati mbaya sana, utaratibu wa kuwapa tahfifu hiyo ya nauli kwa wanafunzi na watoto wa umri usiozidi miaka 18 hapa Zanzibar unaonekana kusuasua ukitilia maanani kwamba kundi la watoto na kundi la wanafunzi (wakiwemo wa vyuo) hayana njia ya kujiingizia kipato kisheria na kimazingira.

(a) Je, Serikali imetoa maelekezo gani kwa vyombo vya usafirishaji kuhusiana na nauli za watoto na wanafunzi na utekelezaji wake ukoje.

(b) Kwa kuwa umri wa mtoto unaotambulika kisheria ni miaka 18, je, ni kwa misingi na miongozo ipi inayolazimisha watoto wa miaka 12 na kuendelea au watoto walio na vimo virefu kukatiwa tiketi ya mtu mzima wanaposafiri.

(c) Je, ni muongozo upi wa sasa unaotumika kuhusu nauli kwa watoto wanaopanda gari za abiria, bajaji na

bodaboda kwenda skuli.

**Wizara ya Afya:**

75. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna taarifa kuwa katika Divisheni ya Afya ya Akili ya Hospitali ya Kidongo Chekundu, kuna uhaba wa watendaji hususan wataalamu bingwa, na kuwepo kwa asilimia kubwa ya watendaji wa mkataba katika divisheni hii wanaolipwa na wafadhili.

(a) Je, kuna ukweli gani wa taarifa hii.

(b) Je, Wizara yako imechukua hatua gani katika kuondosha tatizo hilo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

27. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Skuli ya Dkt. Salim Ahmed Salim iliyopo Wara/Wawi ipo nje kidogo ya makaazi ya watu na hivyo kupelekea changamoto hasa kwa wanafunzi wa kike wakati wa kwenda na kurudi skuli.

Je, ni lini Serikali itajenga dahalia katika skuli hiyo ili kuondosha usumbufu kwa vijana hao.

42. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha vyuo mbali mbali nchini, ikiwa ni pamoja na Chuo cha Afya Mbweni, ingawa Chuo hiki kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wahadhiri.

(a) Je, Wizara yako imekaa lini na Wizara ya Afya pamoja na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), kujadili changamoto hii hasa ikizingatiwa kuwa, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina madaktari wengi wanaoweza kuwa walimu wa Chuo cha Afya Mbweni.

(b) Je, ni lini Serikali italiangalia kwa umakini suala hili kwa kuandaa utaratibu mzuri utakaotumika kwa madaktari hao kufundisha katika Chuo cha Afya Mbweni kama wanavyofanya katika Chuo cha Muhimbili bila ya kuathiri nafasi zao.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

73. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Jengo la Kamisheni ya Ardhi liliopo Wawi Pemba, liko katika mazingira hatarishi sana hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa dharura katika kulihami jengo hilo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
24 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA**